# KISWAHILI PP3 FINAL GAUGE PREDICTION

# ALL SUBJECTS ARE NOW AVAILABLE

**TOPLIGHT PUBLISHERS KENYA 2023 PANEL WORK**

THIS GAUGE SERIES EXAM IS TO DETERMINE CANDIDATE STRENGTH

**THIS EXAMS WAS PREPARED BY 10 EXAMINERS**

**THIS EXAM IS DIRECTED TO ALL KENYAN STUDENTS**

**BECAUSE IT IS TO DETERMIN/PREDICT THE STUDENT FINAL SCORE**

**THIS EXAM MARKING SCHEME WONT BE FREE USE MARKING SCHEME WELL TO CORRECT YOURSELF WELL AND BE FULL PREPARED TO FACE THE NATIONAL EXAMINATIONS WITHOUT ANY FEAR BUT WITH CONFIDENT**

IN RESPONSE TO HIGH TAXES,COST,LABOUR AND SUCH MORE TAXES

MARKING SCHEME FOR THIS PDF (THIS 5 SERIES) GOES @**750**

ALL PAYMENTS SHOULD BE PAID TO OUR:

TILL NO:**8264076**

NAME TOPLIGHT PUBLISHERS KENYA

FOR MORE CALL SIR ABRAHAM **0729125181**

OR

EMAIL;toplightpublisherskenya@gmail.com

# YOURS FAITHFULLY TOPLIGHT'

# KISWAHILI PP3 GAUGE PREDICTION 2023

**NAME…………………………………………………..ADM………………….**

**SCHOOL……………………………………………...INDEX………………**

**DATE………………………SIGN………………………TARGET……………**

**KARATASI YA 3**
**FASIHI**
**KIDATO CHA NNE**

**MUDA: SAA 2 ½**

# GAUGE 1 2023 KCSE PREDICTION

*MAAGIZO:*

a) Jibu maswali manne pekee.
b) Swali la kwanza ni la lazima.
c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani; Riwaya,Ushairi, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.
d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
e) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili
f) Karatasi hii ina kurasa 7 zilizopigwa chapwa
g) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |



FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

**SEHEMU A: TAMTHILIA: *Bembea ya Maisha* - T. Arege (ALAMA 20)**

1. “Siwezi kuendelea kuishi hivi. Sasa nimekata shauri. Pombe! Umenichezesha kama mwanasesere kwa muda mrefu. Umeninyima fursa ya kuielewa familia yangu. Hapana! … Lazima nimshukuru kwa vitendo kwa jinsi alivyojitolea kuijenga familia yetu…kwa heri pombe. Buriani.”

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

b) Eleza vipengele vinne vya kimtindo alivyotumia msemaji kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe. (alama. 4)

c) Fafanua changamoto ya asasi ya ndoa kwa kuangazia ndoa zilizo katika tamthilia ya *Bembea ya Maisha*. (alama 4)

d)"...Wakati mwingine mwindaji huwa mwindwa. Hata kijijini wanaishi watu. Watu hao hawakumbwi na dhiki kiasi hiki. Ya nini kung'ang'ana kuyatafuta maisha kama kwamba hayapiti? Maisha ni mshumaa uso mkesha! Ukijiachia sana peupe hata upepo unaweza kuuzima kabla ya kulika hadi nchani.”

Eleza umuhimu wa msemaji katika kuendeleza ploti ya tamthilia hii. (alama 8)

**SEHEMU B: RIWAYA, - A Matei: Chozi la Heri**

Jibu swali la 2 au la 3

2. Jadili ufaafu wa anwani ya riwaya ya *Chozi la Heri* (alama 20)

3. “…huenda tusikutane nikiwa hai ila nawausia kwa kauli moja tu, msiache ubinafsi na tamaa kuupweza ubinadamu wenu.

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

b) Eleza jinsi ubinafsi na tamaa ulivyopweza ubinadamu wa wahusika kwa mujibu wa riwaya ya *Chozi la Heri*. (alama 8)

c) Kwa kurejelea Pete na Shamsi, jadili mchango wa wahusika hawa katika kujenga maudhui.

(alama 8)

**SEHEMU C: USHAIRI**

*4.* ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

***Timothy Arege – Mwili***

Leo kitaka nifike, natamani, ila wauma mwili
Kwa kazi nihusike, samahani, unahili kimwili
Napenda nihesabike. makundini, ila huwezi mwili.

Vitisho pamwe kelele, ninavicha, kwa nafsi na mwili
Ila ugonjwa utimile, umechacha, na kuudhili mwili
Msikose simile, magalacha, si gurudumu mwili.

Vingekuwepo viraka, kuutia, ngeushuruti mwili
Kifundi kuvipachika, kuingia, hata kuridhi mwili
Upya ukaungilika, kuvutia, roho na wake mwili.

Lakini kamwe haiwi, kuvipata, vipande vyake mwili
Sihofu kupata mawi, sitajuta, kupigania mwili
Hata kufutwa sikawi, nitakita, kidete nao mwili

Kazi ninaithamani, ni hakika, akilini na mwili
Ila kamwe siamini, kusagika, damu jasho na mwili
Uwele hususani, kioneka, nguvu hitishi mwili

***Maswali***

a) Fafanua mambo ambayo mtunzi anasisitiza katika shairi hili. (alama 8)
b) Bainisha mbinu nne ambazo mtunzi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika shairi. (alama 4)
c) Eleza toni ya shairi. (alama 2)
d) Tambua nafsi nenewa na nafsi neni katika shairi hili ( alama 2)
e) Bainisha bahari ya shairi hili kwa kurejelea vipande. (alama 1)
f) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari. (alama 3

5. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

KAMA SODOMA!
Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Haihitaji makini, kwa mwenye macho mazima
Utaona walakini, mradi ukitizama
Wanazini hadharani, wana kwa watu wazima


FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Wanazini hadharani, wana kwa watu wazima
Wanatafuna maini, vijana na kina mama
Hawana haya nyusoni, wameharamisha wema
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Hawana haya nyusoni, wameharamisha wema
Baba na binti ndani, wanacheza lelemama
Marijali wa mbioni, kujipagaza umama
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Marijali wa mbioni, kujipagaza umama
Wameikataa dini, toka tumboni mwa mama
Wadai wataliani, watajirisha mapema
Yafanana na sodoma, mji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Wadai ufirauni, watajirisha mapema
Hivyo mambo ya kigeni, yametunukiwa dhima
Uwaonapo fuoni, nusu uchi wa mnyama
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Uwaonapo fuoni, nusu uchi wa mnyama
Watu hawana imani, umezidi uhasama
Na viongozi wa dini, kuabudu darahima
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Na viongozi wa dini, kuabudu darahima
Wamekeuka yamini, kati yao na Rahima
Wamemuasi Manani, na kusahau kiyama
Yafanana na sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Wamemuasi manani, na kusahau kiyama
Ya Illahi tuauni, tuwe watu maamuma
Tukue katika dini, siku zetu za uzima
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

MASWALI

(a) Bainisha bahari ya shairi hili ukijikita katika ruwaza zifuatazo (alama 3)



FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

i) Mishororo
ii) Maneno
iii) Vina

(b) Eleza muundo wa shairi hili (alama 4)
(c) Bainisha mbinu zifuatazo za kimtindo katika shairi hili (alama3)
i) Tashbihi
ii) Taswira
iii) Tasfida

(d) Eleza toni ya shairi hili (alama1)
(e) Bainisha nafsi nenewa katika shairi hili (alama 1)
(f) Fafanua dhamira ya mtunzi wa shairi hili (alama 2)
(g) fafanua ujumbe wa shairi hili (alama 4)
(h) Fafanua maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa na mshairi (alama 2)
i) Manani
ii) Marijali

**SEHEMU YA D: Hadithi Fupi – Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine – Dw Lutomia**

6. "Poko! Ukiumwa na nyuki haina haja ya kujitwika jukumu la kuharibu mizinga yote ya asali. Hujui faida ya nyuki ulimwenguni? Uliamua kuharibu asali ya nchi. Jadili maudhui ya ukiukaji wa haki za watoto katika hadithi ya ;

i. Mapambazuko ya Machweo (alama 10)
ii. Sabina (alama 10)

7. Siku moja alipokataa katakata kuandamana na mumewe, jungu lilifoka. "Wewe mke sampuli gani usiyetaka kumuunga mkono mmeo?" Haya kaa nyumbani. Kula na kulala tu, hujui jingine. Ona umbo lako sasa, kama nguruwe. Si mke mrembo niliyeoa! Wanawake ni wengi…"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
c) Bainisha vipengele vinne vya kimtindo katika dondoo hili (alama 4)
e) Fafanua nafasi ya mwanamke katika hadithi hii. (alama 12)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

8. Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali


FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

Hapo zamani za kale, Nyani na Mamba walikuwa marafiki wa kufa kuzikana. Watoto wao walipendana na kufaana kama ndugu wa toka nitoke. Familia ya Mamba aliishi mtoni nayo ya Nyani aliishi katika msitu uliokuwa maili thelathini kutoka mtoni. Kila mara marafiki hawa walitembeleana na kusaidiana kwa hali na mali. Kwa vile Mamba alikuwa mvuvi mashuhuri, aliweza kumwauni Nyani na aila yake kwa samaki wa aina mbalimbali. Nyani naye alimpelekea Mamba matunda na nafaka kutoka shambani mwake.

Urafiki wao ulikita mizizi na kunawiri zaidi wakati Mamba alipokuja kwa Nyani kumposea mwanawe binti. Ukwe uliutilia viungo uhusiano wa Nyani na Mamba wakawa wanagandana kama kupe na mkia wa ng'ombe. Wakatenda mengi pamoja. Wakazungumza ya kupwa na ya kujaa. Hakuna hata mmoja wao aliyeutilia shaka uaminifu wa mwenzake. Wake zao nao walifuata kaida ya maji kufuata mkondo. Walikuwa masahibu wa chanda na pete.

Msimu mmoja wa mapukutiko ulishuhudia mabadiliko ya kudumu katika maisha ya Nyani na Mamba. Wakati huo, bahari ilichafuka si haba. Kazi ya Mamba ya uvuvi ikaanza kukabiliwa na majabali ya kila aina. Kila mara Mamba alipokwenda uvuvini, alirudi akichekelewa na nyavu zake. Hakuambulia chochote. Njaa ilianza kubisha hodi katika familia ya Mamba. Hali hii ilitishia kuutia ufa urafiki kati ya Mamba na Nyani. Mamba alivamiwa na pepo ambaye hata yeye alishindwa kumfahamu. Kila mara alipomwona. Nyani au watoto wake alitamani kumdakia na kumla mzima mzima. Kadiri alivyojaribu kujiasa dhidi ya fikira hii mbovu ndivyo moyo wake ulivyoendelea kumshauri, "Una njaa bwana, familia yako itaangamia. Je huoni rafiki yako na familia yake wanaweza kuwa kitoweo? Utaendelea kula wishwa hadi lini? Mbona huyo Nyani ambaye anajiita rafiki yako sasa amekata guu humu? Mbona haji tena kukutazama? Hata karafuu alizokuwa akikuletea ameacha kuleta. "Mamba akaanza kumshuku rafiki yake na akasadiki kuwa Nyani alikuwa mla naye tu.

Usiku mmoja baada ya kula mate na kujilaza kitandani mwake akihesabu nyota, wazo lilimjia. Alikata shauri kumlaghai rafiki yake wa miaka mingi ili apate kujiokoa yeye na familia yake kutoka katika kinamasi cha njaa. Asubuhi yake alikwenda kwa Nyani akiwa amejiinamia kwa jitimai. Alisema, "Rafiki yangu, jana tulipoagana nilipata tanzia. Mjumbe kutoka kijijini aliniarifu kuwa baba yangu ni mgonjwa mahututi. Alisema kwamba baba ananitaka nyumbani upesi," Habari hizi zilimtia Nyani majonzi makuu. Alimwahidi Mamba kwamba wangeandamana pamoja. Kwa vile Nyani hangeweza kutembea majini, ilibidi abebwe na Mamba. Alipatwa na kichefuchefu na manyezi kila alipotazama bahari iliyojitandaza mbele yao kwa mbwembwe. Hata hivyo,


FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

Mamba alimhakikishia kuwa wangefika salama. Naye kwa Imani iliyotokana na urafiki na mazoea ya miaka mingi, alitulia.

Safari ilikuwa ndefu na yenye machovu yaliyomfanya Nyani kulala mgongoni mwa Mamba. Walipofika kwenye vina vya maji, Mamba aliamua kumpasulia mbarika Nyani. “Rafiki yangu, nimekuwa nikidhani wewe ni rafiki wa dhati, kumbe uzuri wako wa mkakasi? Mimi na wanangu tumetafunwa na njaa kwa miezi kadha sasa huku maghala yako yakishiba na kutapika chakula. Hujadiriki hata siku moja kuja kujua kama nimepata hata senti moja ya kusagia mkunguni. Jana usiku nilipokuwa nikiwazia hali yangu, nilioteshwa katika ndoto kwamba kama ningepata moyo wako na kuula, basi hali ya uhitaji ingeniishia. Moyo wangu unaniuma sana kukufanyia tendo hili, hata hivyo lisilo budi hutendwa.”

Nyani alipigwa na butwaa nusura moyo wenyewe ujikabidhi kwa Mamba. Hata hivyo, akili yake nyepesi ilifanya kazi. Alimwambia Mamba,”Ndugu yangu, pole sana ikiwa umekuwa unadhani sikujali. Kwa kweli, hata ungeniomba moyo wangu siku hizo ningekupa tu. Unajua tena sisi Nyani, Tumbili na Kima tuna mioyo mingi. Hata hivyo, nasikitika kuwa Mungu alituambia kuwa daima mioyo yetu itakaa mitini. Basi ndugu mpenzi, badala ya kuendelea na safari hii, turudi pale mtini nikupe moyo wangu pamoja na mitatu ya wanangu kusudi uwalishe wanao na mkeo.”

Mamba akaingia mtegoni. Wakarudi hadi ufuoni. Kwa vile Mamba hakuweza kutoka majini, alibaki ufuoni akimngojea rafiki yake amletee mioyo.

Mamba alitunga macho yake kwenye ujia alioufuata Nyani akiomba pasitokee lolote la kumcheleweshaNyani. Matumbo yalimnguruma kwa njaa. Roho ikampapa kwa tumaini. Alingoja, akangoja, akangoja... wiki, mwezi, mwaka... Nyani hakurudi. Mamba akajua amepwaguliwa na Nyani. Akaapa kumtafuta kwa udi na ambari. Huo ukawa mwisho wa urafiki kati ya Nyani na Mamba. ***Hadithi yangu inaishia hapo.***

Maswali

a) Tambua kipera cha utungo huu. Thibitisha. (alama 2)

b) Fafanua mbinu sita za kimtindo alizotumia mtambaji wa utungo huu. (alama 6)

c) Jadili shughuli za kiuchumi na shughuli za kijamii katika jamii hii. (alama 4)

d) Umepewa jukumu la kutamba ngano hii. Fafanua mambo manane muhimu utakayozingatia ili kufanikisha uwasilishaji wako. (alama 8)


FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

# KISWAHILI PP3 GAUGE PREDICTION 2023

**NAME………………………………………………………..ADM…………………..**

**SCHOOL……………………………………………………...INDEX………………**

**DATE………………………..SIGN………………………..TARGET……………**

**KARATASI YA 3**
**FASIHI**
**KIDATO CHA NNE**

**MUDA: SAA 2 ½**

# GAUGE 2 2023 KCSE PREDICTION

*MAAGIZO:*

h) Jibu maswali manne pekee.
i) Swali la kwanza ni la lazima.
j) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani; Riwaya,Ushairi, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.
k) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
l) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili
m) Karatasi hii ina kurasa 7 zilizopigwa chapwa
n) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

## SEHEMU YA A

**Swali la lazima**

**1. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo;**

Sinisumbue akili, nakusihi e mwandani,
Afiya yangu nidhalili, muno nataka amani,
Nawe umenikabili, nenende sipitalini,
Sisitoke aazali, twenda zetu mizimuni,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani!

Mababu hawakujali, wajihisipo tabani,
Tuna dawa zaasili, hupati sipitalini,
Kwa nguvu yakirijali, mkuya tiuamini,
Kaafuri pia kali, na dawa ya ndwele fulani,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani!

Mtu akiwa halali, tumbo lina walakini,
Dawa yake ni shubili, au zogo huauni,
Zabadi pia za hali, kwa maradhi yako ndani,
Au kwenda wa sahili, wenyewe walo pangani,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani!

Mtu kwenda sipitali, nikutojuwa yakini,
Daktari kuona mwili, ta nena kansa tumboni,
Visu viti wemakali, tayari kwa pirisheni,
Ukatweka mafigili, tumbo nyangwe na maini,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani!

Japo maradhi dhalili, kuteguliwa tegoni,
Yakifika sipitali, huwa hayana Kifani,
Waambiwa damu kalili, ndugu msaidieni,
Watu wa kitamali, kumbe ndio buriani,
Nifuateni sipitali, na dawa ziko nyumbani!


FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

Mizimu ya kupa kweli, wakueleze undani,
Maradhiyo ni ajali, yataka vitu dhamani,
Ulete kuku wawili, wamanjano wakijani,
Matunda pia asali, vitu vya chanoni,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani!

**Maswali**

a. Lipe shairi hili anwani mwafaka. (alama 2)
b. Liweke shairi hili katika bahari mbili. (alama 2)
c. Andika ubeti wane kwa lugha nathari. (alama 4)
d. Kwa nini mshairi anakataa kwenda hospitali? (alama 2)
e. Ni nani nafsineni katika shairi hili? (alama 1)
f. Tambua toni ya shairi hili. (alama 1)
g. Eleza muundo wa ubeti wa pili. (alama 4)
h. Eleza jinsi uhuru wakishairi ulivyotumi kakatika shairi hili. (alama 2)
i. Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi. (alama 2)
   1. Pangani
   2. Nenende

## SEHEMU YA B: HADITHI FUPI: MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE.

2. "Yu wapi kiruka njia wako? Wajua yuko wapi? Uliacha mbachao kwa msala upitao. Atakutunza nani, maana kwako fadhila zapunda ni mashuzi!"

a. Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)
b. Taja mbinu mbili za lugha zilizotumika katika dondoo hili. (alama 2)
c. Bainisha toni ya dondoo. (alama 1)
d. Fafanua sifa zozote tatu za mzungumziwa.(alama 3)
e. Kwa kurejelea hadithi "Fadhilazapunda" onyesha ukweli wa kauli kuwa fadhila za punda ni mashuzi kwa mifano mwafaka. (alama 10)

**Au**

3. Huku ukirejelea hadithi zifuatazo tano jadili maudhui ya migogoro kwa kutoa mifano maridhawa. (alama 20)
   a) Fadhila za punda
   b) Msiba wa kujitakia
   c) Mapambazuko ya machweo


FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

d) Harubu ya maisha

## SEHEMU YA C: RIWAYA YA CHOZI LA HERI

4. “Kisa cha kaniki cha usiku wa manane kimetanda. Anayetazama anamwona mja aliye vaa koti kuukuu…..Anaimba huku ameshika chupa mkononi…..”

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Tambua aina nne za taswira zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)
c) Fafanua maudhui yanayo changiwa na mrejelewa huku ukirejelea riwaya. (alama 8)
d) Eleza sifa nne za mrejelewa(alama 4)

5. Changanua kifungu kifuatacho.

Mkuu wa shule, walimu na wanafunzi wenzangu, suala la uhifadhi wa mazingira ni jukumu la kila mmoja wetu. Tumeona jinsi misitu ilivyo vamiwa na viongozi wenye mate ya fisi. Naskia baadhi ya vinara wa taasisi mbalimbali za umma wamewaacha wanyama kama mayatima kwa kupoka makazi yao. Maelfu ya maekari ya misitu yamefyekwa nakujengwa viwanda. Badala ya mibambakofi na miti mingine inayo safisha hewa, michai imetwaa nafasi yake. Wanao husika na matendo haya wanapoulizwa hudai kuwa michai si adui wa mazingira! Wengine wanasema kuwa misitu haina budi kukatwa ili kupanda mimea inayotoa chakula, kwani jamii sharti ijitosheleze kwa chakula.

iii. Changanua mtindo katika kifungu kifuatacho. (alama 10

(b)Mbali na maswala yanayojitokeza katika kifungu, eleza namna mwandishi alivyo shughulikia uharibifu wa mazingira katika riwaya ya chozi la heri.

(alama6)

c)Jadili mchango wa vijana katika kubomoa jamii katika riwaya ya chozi la heri.

(alama 4)

## SEHEMU YA D: TAMTHILIA YA BEMBEA YA MAISHA

“Mwanangu binadamu mchoyo kwa lake lakini mkarimu ajabu kwa la mwenziwe.Atakukarimu kwa la mwenziwe na atakupa nyongeza usio hitaji lakini lake atalizika katika giza la kina cha moyo wake. Ndiyo hulka yake mwana wa adamu.”

a. Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
b. Jadili namna chanya msemaji na wenzake wa jinsia ya kike walivyosawiriwa katika tamthilia ya Bembea ya maisha. (alama 6)
c. Fafanua umuhimu wa mazungumzo kati ya msemaji na msemewa katika tamthilia ya Bembea ya Maisha(alama 10)

6. Jadili maudhui yafuatayo kwa kutolea mifano maridhawa kama yanavyoshughulikiwa katika tamthilia ya Bembea ya maisha.(alama 20)
   (a) Mabadiliko
   (b) Migogoro

## 7. SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

Dunia hii ina matatizo x2
Watu wengi hawaja jua
Ni dunia ya taabu
Hata hivyo usijali.

Karibu malaika karibu x2
Mimi nikukaribishe
Kwa mikono yote miwili
Dunia mti mkavu.

Usilie mtoto usilie x2
Kwa kuiona dunia
Iliyo na masumbuko
Umebebwa miezi tisa.

**Maswali**

a. Huu ni wimbo wa aina gani? (alama 1)
b. Eleza ujumbe wa wimbo huu. (alama 2)
c. Eleza sifa za nyimbo za bembea. (alama4)
d. Taja tanzu kuu nne za fasihi simulizi.(alama 4)
e) Unanuia kukusanya data za kipera kilicho hapo juu. Pendekeza njia tano utakazotumia. (alama 5)
f) Eleza changamoto nne utakazo kumbana nazo katika kukusanya data zako. (alama 4)


FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

# KISWAHILI PP3 GAUGE PREDICTION 2023

**NAME……………………………………………………..ADM………………….**

**SCHOOL……………………………………………….....INDEX………………**

**DATE……………………….SIGN………………………..TARGET……………**

**KARATASI YA 3**
**FASIHI**
**KIDATO CHA NNE**

**MUDA: SAA 2 ½**

# <u>GAUGE 3 2023 KCSE PREDICTION</u>

*MAAGIZO:*

g) Jibu maswali manne pekee.
h) Swali la kwanza ni la lazima.
i) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani; Riwaya,Ushairi, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.
j) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
k) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili
l) Karatasi hii ina kurasa 7 zilizopigwa chapwa
m) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |



FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

**SEHEMU YA A:** ***Mapambazuko Ya Machweo Na Hadithi Nyingine- Clara Momanyi***

**SWALI LA LAZIMA**

**1.** "Mike! Mike! Mike! Njoo! Nilijua utafanya vyema mwanangu…"

iv. Tambua na ueleze **toni** ya dondoo hili. (alama 2)
v. Changanua mtindo katika dondoo hili. (alama 2)
vi. Eleza sifa **nne** za msemaji wa dondoo hili. (alama 4)
vii. Eleza mbinu **mbili** ulizozitumia kutambua sifa za msemaji wa dondoo hili. (alama 4)
viii. Tambua na ufafanue madhila yanayomsakama mhusika mkuu katika hadithi hii ya *"Sabina"*. (alama 8)

**SEHEMU YA B: RIWAYA**

***Chozi La Heri-Assumpta K. Matei***

***Jibu swali la 2 au 3***

**2.** "Ndivyo tunavyoishi…na usidhani ni kuishi huku…ni kupapatika, kufufurishwa na matumbwe ya maisha…pole ndugu, itabidi usahau mswala kwa hii mbacha."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Andika mifano **mitatu** ya sitiari katika dondoo hili. (alama 3)
(c) Fafanua umuhimu wa anayeambiwa maneno haya katika kuijenga riwaya hii. (alama 3)
(d) Kwa kurejelea hoja **kumi** za yule anayezungumza, onyesha jinsi raia wa Wahafidhina wanavyopapatika na kufufurishwa na matumbawe ya maisha. ( alama 10)

**AU**

**3**. "Lakini…

Wewe hushangai?

Kwani wanawashwa

Na pilipili iliyo

Kwenye uchango wa mwingine?

Kwani wasitake kukuli

Kilichotufanya mimi na wewe

Kuwa marafiki wa kufa kuzikana?"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Tambua mbinu **mbili** za kimtindo katika dondoo hili (alama 2)

(c) Eleza sifa **nne** za msemaji wa maneno haya. (alama 4)

(d) Jadili vyanzo na athari za matumizi mabaya ya vileo na dawa za kulevya kwa mujibu wa diwani ya Chozi la Heri huku ukitolea mifano mwafaka. (alama 10)

## SEHEMU YA C: TAMTHILIA

***Bembea ya Maisha- Timothy Arege***

***Jibu swali la 4 au 5***

**4**."…anachukua vidonge vyake na kuvimeza kabla ya kuketi kwenye kochi mpya."

d. Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
e. Tambua aina za taswira katika dondoo hili. (alama 2)
f. Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo hili. (alama 4)
g. Eleza nafasi ya mwanamke ukijikita katika utamaduni wa jamii ya *"Bembea ya Maisha"*. (alama 10)

**AU**

**5**. " Wakati mwingine maisha haya hukufanya kijisikia kama abiria kwenye gari liendalo kwa kasi. Unatamani dereva apunguze mwendo lakini unakumbuka kuwa safari bado ni ndefu na hutaki kufika ukiwa umechelewa. Basi unatulia japo ndani una wasiwasi, hutulii. Lakini huwezi kushuka maana safari itaganda. Kwa hivyo, unajitahidi tena, japo wakati mwingine unajikuta umetambaliwa na uchovu, shaka na tuhuma."

(a) (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Changanua mtindo katika dondoo hili. (alama4)
(c) Dhihirisha umuhimu wa mzungumziwa wa maneno haya katika kuijenga tamthilia ya *"Bembea ya Maisha*". (alama 6)
(d) Eleza namna maisha yanamfanya mzungumzaji "kujisikia kama abiria kwenye gari liendalo kwa kasi".(alama 6)


FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

**SEHEMU YA D: USHAIRI**
***Jibu swali la 6 au 7***

6. ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

Jama, Jama, Jamani
Mbona twabebeshwa mateso hivi
Mizigo mikubwa ya dhiki kama
Kwamba hatuna haki ya kusema
Kukataa ndoa za lazima
Kukataa kuozwa wazee
Kukataa kukatishwa masomo
Kukataa tohara ya lazima

Jama, Jama Jamani
Iweje tuteswe mateso haya
Na watu wasio kuwa hata na haya kama
Kwamba hatuna haki ya kulalamika
Kulalamikia kutumikishwa kama mayaya
Kulalamikia kudhalilishwa kiunyama
Kulalamikia kutolindwa na sheria

Jama, Jama, Jamani
Sasa hii ni awamu nyingine
Na macho tumeyafungua kabisa
Tumekataa kudhalilishwa kabisa
Tumekataa kuteswa kama watumwa
Tumekataa tohara ya lazima
Tumekataa kuozwa....... Tumekataa! Tumekataa
Hii awamu ya 'Haki ya mtoto wa kike'

**<u>Maswali</u>**

(a) Taja mambo **matatu** muhimu yaliyozungumziwa na mshairi kisha ueleze kila moja . (alama 6)

(b) Eleza muundo wa shairi hili (alama 4)

(c) Taja mbinu **mbili** za lugha alizotumia mshairi kisha ueleze kila moja (alama 4)

(d) Kwa nini mshairi huyu anasema hii ni 'awamu' nyingine? (alama 3)

(e) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa na mshairi (alama 3)

f. awamu
g. kudhalilishwa
h. Dhiki

**AU**

**7. <u>Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo</u>**

a. Mkata ni mkatika, harithi hatoridhiwa
Sina ninalolishika, wala ninalochukuwa
<u>Mlimwengu</u> <u>kanipoka,</u> hata tone la muruwa!
Mrithi nini wanangu?

b. Sina ngo'mbe sina mbuzi, <u>sina konde sina buwa</u>
Sina hata makaazi, mupasayo kuyajuwa
Sina mazuri makuzi, jinsi nilivyoachwa
Mrithi nini wanangu?

c. Sina kazi sina bazi, ila <u>wingi wa shakawa</u>
Sina chembe ya majazi, mno nikukamuliwa
Nakwa'cheni upagazi, ngumu kwenu ku'tuwa
Mrithi nini wanangu?

d. Sina sikuachi jina, mkata hatasifiwa
Hata nifanye la mana, mno mi kulaumiwa
Poleni wangu sana, sana kwenu cha kutowa
Mrithi nini wanangu?

e. Sina leo sina jana, sina kesho kutwaliwa
Sina zizi sina shina, wala tawi kuchipuwa
Sina wanangu mi sina , sana la kuacha kuraduwa

Mrithi nini wanangu?

f. Sina utu sina haki, mila yangu meuliwa
Nyuma yangu ili dhiki, na mbele imekaliwa
N'nawana na miliki, hadi nitakapofukiwa
Mrithi nini wanangu?

g. Sina ila kesho kwenu, wenyewe kuiongowa
Muwane kwa nyinyi mbinu, mwende pasi kupumuwa
Leo siyo kesho yenu, kama mutajikamuwa
Mrithi nini wananngu?

i. Taja mambo yoyote **mawili** ambayo mtunzi angewarithisha wanawe. (alama 2)

ii. Eleza sababu ya mtunzi kutoweza kuwarithisha wanawe. (alama 3)

iii. Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari. (alama 4)

iv. Dondoa mifano **miwili miwili** ya : (alama 2)

a. Inkisari

b. Tabdila

v. Chambua shairi hili kwa upande wa :

1. Dhamira (alama2)

2. Muundo (alama 4)

vi. Eleza maana ya vifungu vifuatavyo kama vilivyotumiwa katika shairi. (alama 3)

a. Mlimwengu kanipoka

b. Sina konde sina buwa.

c. Wingi wa shakawa.

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

**h. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.**

Malaika
Nakupenda malaika x2
Ningekuoa malaika...
Ningekuoa dada...
Nashindwa na mali sina wee...

Ningekuoa malaika x2

Pesa, zasumbua roho yangu x2


FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

Nami niafanyeje, kijana mwenzio
Nashindwa na mali sina wee...

Ningekuoa malaika x2

e) Ainisha wimbo huu kwa kuzingatia kipengele cha maudhui. (alama 2)
f) Andika sifa **mbili** za jamii inayosawiriwa na wimbo huu. (alama 2)
g) Eleza mikakati **sita** ambayo mwimbaji angetumia kufanikisha uwasilishaji wa wimbo huu. (alama 6)
h) Unanuia kutumia mahojiano kukusanya habari kuhusu nyimbo za aina hii.
   j. Eleza manufaa **matano** ya kutumia mbinu hii. (alama 5)

   k. Eleza changamoto **tano** za kutumia mbinu hii. (alama 5)


FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

# KISWAHILI PP3 GAUGE PREDICTION 2023

**NAME……………………………………………………..ADM…………………..**

**SCHOOL…………………………………………………INDEX………………**

**DATE……………………….SIGN………………………..TARGET……………**

**KARATASI YA 3**
**FASIHI**
**KIDATO CHA NNE**

**MUDA: SAA 2 ½**

# GAUGE 4 2023 KCSE PREDICTION

*MAAGIZO:*

n) Jibu maswali manne pekee.
o) Swali la kwanza ni la lazima.
p) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani; Riwaya,Ushairi, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.
q) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
r) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili
s) Karatasi hii ina kurasa 7 zilizopigwa chapwa
t) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |


FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

**SEHEMU A: USHAIRI**

**1. LAZIMA**

T. Arege: Wimbo wa Kichaa

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Bustani za jadi
Maua ya kuchezea vipepeo
Na pua kufurahisha
Sasa ni mabaki ya kumbukumbu
Za yaliyojiri hapa
Na kukiacha Kijiji kinywa wazi.

Hapa walimpiga mwereka
Dada yangu; mdogo wangu
Shuleni akitoka
Na mkoba wa kilo nzito za vitabu
Chini akakandamiziwa
Wakachana mbuga na wake ubikira!

Pale kando ya mto
Walimvizia na kumburura shangazi
Binamu zangu wadogo wakiona
Marinda wakamchania
Kabla ya kumtia kidonda shangazi
Naye ami kumchania kovu moyoni!


FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

Ni hapa kando ya barabara kuu
Ambapo nyanyangu walimshika mkono
Uchochoroni wakamburuta
Na kumfanya kujutia
Bahati mbaya ya kuishi kwingi
Akaganda uchochoroni
Hadi alipoletwa nyumbani kesho yake
Na wachungaji wa muchungani.

Si hapa walipomshurutisha mama
Chini wakamkanyagia
Kama kuku wa kuchinja
Baada ya yake sidiria kuikata?
Si hapa sebuleni mwetu?
Si hapa sokoni
Nilipopata vazi la stara
La wangu mke mpendwa
Lilikatwa yake mihimili?

Yule kichaa wa mwetu sokoni.
Akawa kichwani amelivaa
Na kuimba wimbo wa maombolezi
Huku wanakijiji wakimpuuza
Na watoto kumcheka?

Ni hapa ambapo usiku ulipoingia
Hawakusita kuhakikisha kuwa

Yule kichaa amewazalia mtoto

Na kujitia kundini kushangaa

Kilichomtuma atake kujifungua!

**Maswali**

i) Tambulisha **nafsineni** katika shairi hili. (alama 2)
j) Eleza **dhamira** ya mshairi. (alama 2)
k) Fafanua mbinu za **kimtindo** zinazojitokeza katika shairi hili. (alama 5)
l) Eleza aina za **taswira** zinazojitokeza katika shairi hili. (alama 4)
m) Bainisha **toni** ya mshairi. (alama 2)
n) Onyesha matumizi ya **mishata** katika shairi hili. (alama 1)
o) Fafanua **muundo** wa shairi hili. (alama 4)

## SEHEMU B: RIWAYA

**A.MATEI:** Chozi la Heri

Jibu Swali La 2 au 3

**2. ‘‘Tokeni ! Tokeni kama bado mnataka kuishi!”**

(a) Jadili **umuhimu** wa msemaji wa maneno haya katika kuendeleza ploti ya riwaya hii. (alama 4)

(b) Jadili umuhimu wa **mandhari** haya katika kuendeleza riwaya ya *Chozi La Heri* . (alama 6)

(c) Riwaya ya *Chozi la Heri* imekumbwa na migogoro mingi. Jadili migogoro hii na visababishi vyake. (alama 10)

**3 ‘‘Machozi ya mwanaume hayapaswi kuonekana hata mbele ya majabali ya maisha”**

(a) Eleza majabali ya maisha yaliyomkumba msemewa katika dondoo hili kwa kurejelea riwaya nzima. (alama 10)

b) Kwa kurejelea hoja **kumi** kutoka kwenye riwaya, jadili namna haki za watoto zinavyokiukwa. (alama 10)

## SEHEMU C: TAMTHILIA

**T.M. Arege:** Bembea ya Maisha

Jibu swali la 4 au la 5



FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

**4** a) Changanua **mtindo** katika kifungu kifuatacho (alama 10)

‘‘Mwanangu usitake sana kuhoji alacho kuku. Utachafukwa roho umchukie kuku bure. Wala usitake kujua nyuki ameitengenezea nini asali. Hutaila. Maadamu yameshakuja,yapokee. Mtoto akinyea kiganja hakikatwi wala hatuulizi kwa nini. Ni maumbile. Maumbile hayo,sawa na vidole, hayafanani. Sawa na watoto wachezeao bembea, tumeicheza na tungali tunaicheza sehemu yetu kwa zamu. Haidhuru iwe ya kamba au chuma. Muhimu ni kwamba tumeshirikiana kusukumana kwenye bembea ya maisha. Upo wakati inakuwa raha tele na upo wakati inakatika na kutubwaga. Hiyo ndiyo raha hasa ya maisha. Ni sawa na chombo kinachomenyana na mawimbi katika bahari. Hutufanya kuwa macho katika safari…”

b) Fafanua namna <u>mandhari</u> ya dondoo hili yalivyochangia usukaji wa tamthilia. (alama 10)

5. ‘‘Walishasema baada ya dhiki ni faraja, Faraja ni zao la dhiki. Leo hii kikapu cha mama kimejaa ndago.”

a) Eleza **muktadha** wa dondoo hili. (alama 4)
b) Eleza vipengele **viwili** vya kimtindo kwenye dondoo. (alama 4)
c) Eleza maudhui **mawili** yanayodokezwa kwenye dondoo. (alama 2)
d) Eleza **sifa** za msemaji. (alama 5)
e) Kwa kutolea mifano mwafaka eleza dhiki alizopitia mama ambaye sasa kikapu chake kimejaa ndago. (alama 5)

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

**D.W Lutomia na P. Muthama (Wah):** *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

Jibu Swali la 6 au La 7

6. *R.Wangari*: Fadhila za punda

Anwani ‘Fadhila za Punda’ inaafiki hadithi hii” Thibitisha. (alama 20)

**7.** *W.N Ogeche*: Sabina

a) Changanua mtindo katika dondoo lifuatalo; (alama 6)

‘Athari ya mawazo yake ilijiandika dhahiri shahiri usoni mwake. Alianza kwa kuachia tabasamu pana mithili ya msafiri aliyefika salama. Baada ya dakika chache machozi yalianza kumtoka njia mbilimbili huku kajishika tama. Alifikiria kuhusu mtihani uliodhamiriwa kuanza siku ya Jumanne. Mtihani ambao ungemwezesha kupata ufadhili katika shule ya upili ya bweni ikiwa angepita vyema. Hili ndilo wazo lililozua tabasamu. Lakini, angefeli je?Hatima yake ingekuwa ipi? Maswali haya yalimliza yakamwacha akisinasina kama mgonjwa wa mafua. Akiwa katika

hali hii, aliyakumbuka maneno ya mwalimu mkuu, ‘‘mizizi ya elimu ni michungu ila matunda yake ni matamu. Ikiwa mnataka kuyaonja matunda ya elimu, lazima mtie bidii kwani mtaka cha mvunguni sharti ainame.”

b) Bainisha mbinu **mbili** zinazoweza kutumiwa kutambua sifa za mhusika Sabina kwa kurejelea hadithi *Sabina.* (alama 2)

c) Taja na ueleze aina **mbili** za taswira zinazojitokeza kwenye dondoo hili. (alama 2)

d) Kwa kutolea mifano mwafaka eleza matatizo yanayomkumba mwanamke katika hadithi *Sabina.* (alama 10)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

8(a) Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.

Kila kukicha mashaka

Ni kero hili si huba

Mimi pendo la viraka, heri demu la mkoba

Mimi mno nataka, kuishi nawe muhiba

Pendo viraka viraka

Litanishinda kuziba

Kamwe sitoshughulika

Nawaje wenye kuziba

Viumbe wanosifika, kwa fedha, chuma na shaba

Walostarabika, si mimi wa tobatoba

Pendo viraka viraka

Litanishinda kuziba



FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

Naapa sitojitweka

Limenichosha si haba

Nasomba vyangu viraka, nitie kwenye mkoba

Sikuye ya kuzinduka, mjinga hawi ni juba

Pendo viraka viraka

Litanishinda kuziba

i.Huu ni wimbo wa mapenzi. Thibitisha. (alama 2)

ii.Eleza sifa **mbili** za nafsi nenewa katika wimbo huu. (alama 2)

iii.Fafanua mbinu **tatu** ambazo nafsineni ametumia kufanikisha uwasilishaji wake. (alama3)

iv.Eleza faida **nne** za kurithisha wimbo huu kwa vizazi vijavyo. (alama 4)

(b)Unanuia kufanya utafiti kuhusu utungo wa maigizo :-

(i) Eleza hatua **tatu** utakazofuata katika utafiti wa utungo huu. (alama 3)

(ii) Unanuia kutumia **hojaji** kutafitia utungo huu. Eleza **umuhimu** na **udhaifu** wa kutumia njia hii. (alama 6)

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA**



FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM **0729125181**

# KISWAHILI PP3 GAUGE PREDICTION 2023

**NAME…………………………………………………..ADM…………………..**

**SCHOOL……………………………………………...INDEX………………**

**DATE………………………SIGN………………………..TARGET……………**

**KARATASI YA 3**
**FASIHI**
**KIDATO CHA NNE**

**MUDA: SAA 2 ½**

# GAUGE 5 2023 KCSE PREDICTION

*MAAGIZO:*

u) Jibu maswali manne pekee.
v) Swali la kwanza ni la lazima.
w) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani; Riwaya,Ushairi, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.
x) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
y) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili
z) Karatasi hii ina kurasa 7 zilizopigwa chapwa
aa) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |



FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

**SWALI LA KWANZA;LAZIMA**

**SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI**

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali**

Kijiji chavuma vishindo,
Vya ngoma na nyimbo.

Kwenye vilima vya kata,
Na mabonde kuliko na mito,
Wamama wanalitafuna,
Watoto na vijana wanaliimba, jina,
Jina la nguli Amali wa Jamali. Jamadali kamili.

Ukoo wake wa mashujaa,
Babuze walisifika sana,
Mikuki na mishale walifua,
Kuihami jamii na riaka,
Na hata magao ya kujisitiri, pindi lijapo pambano.

Leo yeye atamba,
Shujaa wa nguvu za tembo,
Mwamba anayepigana bila silaha yoyote,
Angurumapo mahasimu wanazirai, wanavaa lebasi ya woga hasa,
Wasiwasi unawakumbatia.
Angurumapo simba mcheza nani?
Anapotisha Amali wa Jamali atasimama nani?

Zawadi za kole za nazi,
Na mashuke ya mtama,
Zamiminika kwake kutoka kusini na kaskazini,
Kwa kujuhudi za kuwarejesha mitamba na mafahari,
Kutoka mbali walikotekwa,
Mazizi sasa yana uhai,
Miroromo sasa inasikika tena.

Wengine wanaleta vishazi vya samaki,
Kumtunuku,
Huyu mja mwenye nemsi zisizo na ndweo.

Akida wetu,
Atamvisha taji la ngozi ya duma,
Yenye kipembe cha kifaru,
Atamvisha nguo ya ngozi ya simba.

**Maswali:**

l. Tambua kipera cha utungo huu na utoe sababu ya jibu lako. (alama 2)
m. Ni sifa gani hukibainisha kipera ulichotaja hapo juu? (alama5)
n. Mwimbaji ana nafasi muhimu katika uwasilishaji wa nyimbo.Eleza.(alama.5)
o. Jamii iliyoakisiwa kwenye utungo huu huendeleza shughuli gani za kiuchumi? (alama. 4)
p. Fafanua mtindo katika kifungu hiki. (alama.4)

**SEHEMU YA B**
**Riwaya: *Chozi la Heri* - Assumpta Matei**
Jibu swali la *2au3*

**2a)** ``Kumbe hata wewe shemeji..............upo?''
``ndio tu hapa na wengi''
i.Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama.4)
ii."Wengi" wanaorejelewa katika dondoo hili walikumbwa na matatizo yapi?(alama 8)

**b**).``Kule kulazimika kupapasa kwenye giza kutafuta...........''
Mrejelewa katika kauli hii anayafichua maovu yapi katika jamii? (alama.8)

**3.**

**e. Jadili mtindo kwenye dondoo hili. (alama 8)**
Jua linalochomoza halina ule wekundu wa jua la matlai ambao huleta haiba ya uzawa wa siku yenye matumaini. Naona wingu kubwa angani likitembea kwa kedi na madaha na kulifunika jua. Tukio hili linafuatwa na umeme, kisha mtutumo wa

radi. Mawingu yaliyoshiba yakataka kutapika yanagooka, yanakaribiana, kupigana busu na kusababisha mwanguko wa matone mazito ya mvua; matone yanayoanguka kwenye ngozi laini za wanangu wakembe, Lime na Mwanaheri. Nawatazama kwa imani lakini siwezi kuwasaidia. Sina hata tambara duni la kuwafunikia. Linalobaki ni kumshuru Mungu kuwa tungali hai. Ubavuni mwangu amelala maskini mke wangu,Subira. Sijui kama inahalisi kumwita mke wangu kwani huyu siye Subira wangu wa zamani. Siye, siye, siye-e-e-e. Tazama uso wake ulivyovamiwa na majeraha, kikwi. Tazama tambo lake lililoumbuka. Amevimba na kuvimbiana kama dongo la unga ngano baada ya kutiwa hamira. Lakini yeye hana la hamira! Haya ni matokeo ya ubahaimu wa binadamu. Kwa mbali namwona Ridhaa – mwamu hasa – akitafuna kitu fulani, nadhani ni mzizimwitu. Ridhaa, kweli Ridhaa kula mzizi! Daktari mzima! Mkurugenzi mzima wa Wakfu wa Matibabu nchini! Wanasema wajuao kuwa simba akikosa nyama hula nyasi. Msafiri kafiri ati! Amekosa la maama, hili la mbwa ataliamwa!

***b)*** "Huyu hapa ni Bwana Mwangemi na huyu hapa ni Bi Neema. Kama nilivyokujuza hapo awali, wamekuja kuchukukua kwenda kuishi nao kama mwana wao."

(e) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(f) Bainisha mtindo katika dondoo. (alama 3)
(g) Toa sifa za msemaji wa dondoo hili. (alama 5)

## SEHEMU YA C: TAMTHLIA

## PAULINE KEA: KIGOGO

### Jibu swali la 4 au 5

i. "Hata nami naona pengine amenusa sumu."

(c) Eleza muktadha wa dondoo hili. (ala 4)
(d) Eleza ni kwa nini mrejelewa anasemekana kuwa amenusa sumu(ala 2)
(e) Tambua mbinu ya lugha iliyotumika katika dondoo hili. (ala 1)
(f) Mwandishi wa Tamthlia hii amefaulu sana katika matumizi ya mbinu hii uliyotaja hapo juu. Kwa kutoa hoja **saba** thibitisha haya. (ala 7)
(g) Eleza umuhimu wa mzungumziwa (ala 6)

j. "Fungua macho uone. **Keki imeliwa kwingine**, mwaletewa masazo.

p) Eleza muktadha wa dondoo hili. (ala 4)
q) Tambua mbinu ya kisanaa iliyotumika katika dondoo hili (ala 4)


FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

r) Thibitisha kuwa keki imeliwa kwingine (ala 6)
s) Eleza sifa za msemaji wa maneno haya (ala 6)

***SEHEMU YA D: USHAIRI***
***Jibu swali la 6 au 7***
*6.* ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

**SIPENDI KUCHEKA**

Pana jambo natukiya, kwangu hilo muhali,
Kitenda naona haya, kujishusha yangu hali
Sipendi unipe hidaya, sipendi kutenda hili
Sipendi mimi kucheka

Sipendi mimi kucheka, kuchekea mawi
Sipendi na ya dhihaka, kwangu nyemi hiwi
Sipendi kwa hakika, mwovu kistawika
Halafuye nikacheka!

Maskini akiteswa
Yatima akinyanyaswa
Mnyonge naye akinyonywa
Sipendi hata ikiwa
Uwezo nguvu najuwa
Ni hili sitatekezwa
Mbona lakini nicheke, kwayo furaha?
Na wewe ukajiweke, uli na siha?
Na yatima ali pweke, ye anahaha?
Amenyimwa haki yake, hanayo raha!
Na moyo wangu ucheke, kwa ha ha, ha!
Kumbuka kwa kucheka Mimi katu sitacheka.

***Maswali***

bb) Shairi hili ni la aina gani? Thibitisha (ala.3)
cc) Taja sababu zinazomfanya mshairi asitake kucheka. (ala.3)
dd) Chambua umbo la shairi hili kwa kuzingatia ubeti wa mwisho. (ala4.)
ee) Tambua nafsineni na nafsinenewa katika shairi hili. (ala.2)
ff) Tambua toni ya shairi hili. (ala.1)
gg) Fafanua uhuru wa mshairi katika shairi hili. (ala.2)
hh) Eleza aina tatu za urudiaji katika ushairi. (Al.3)
ii) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumka katika shairi


FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

(ala.2)

(i) Mawi

(ii) Nyemi

*7.* ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yatakayofuata.***

Kimya changu kimezidi, navunja yangu subira,
Narejeya miradi, kuhitimisha dhamira,
Kukejeli sina budi, niwafunze utu bora,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Serikali bila hadi, ndo kiini cha madhara,
Yanopiga kama radi, isokuwa na ishara,
Yamini kuwa gaidi, watupora mishahara,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Wamejifanya hasidi, wasopatana fikira,
Wana yao makusudi, kujisombea ujira,
Wakilenga kufaidi, tumbo zao za kichura,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Nchi yetu kufisidi, ni jambo linonikera,
Tangia siku za jadi, ufukara ndo king'ora,
Kutujazeni ahadi, nyie mkitia fora,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Fakiri watozwa kodi, wa pwani na walo bara,
Kwa uvumba hata udi, mwawalipa kwa hasara,
Hamudhamini miradi, mejihisi masogora,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Mesema kazi ni chudi, basi sirikali gura,
Nafsi zenu mzirudi, mkubali kuchakura,
Makondeni mkirudi, muondoe ufukara,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Ujanjenu umezidi, demokrasia bakora,
Debeni takaporudi, michirizi kwenye sura,
Kuwachuja ndo! muradi, kwa za mkizi hasira



FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

***Maswali.***

ix. Toa anwani mwafaka kwa shairi hili. (ala.1)
x. Ainisha shairi hili kwa bahari **tatu** huku ukitoa sababu.(ala.3)
xi. Onyesha mbinu mbili za lugha katika shairi hili. (ala.2)
xii. Eleza mbinu ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi.(Al.3)
xiii. Andika ubeti wa nne katika mtindo tutumbi/nathari. (ala.4)
xiv. Nafsineni analalamikia nini katika ushairi. (ala.3)
xv. Taja mpango mmoja unaotajwa kama njia ya kutatua matatizo ya nchi. (ala.1)
xvi. Eleza muundo wa shairi hili. (ala.3)

**SEHEMU YA E.**
**<u>HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE</u>**

***Jibu swali la nane au la tisa***

**8. Mame Bakari**

"Dunia we' dunia. Dunia ya mwenye nguvu, si ya mimi dhaifu wa nguvu. Dunia ya msumari moto juu ya donda bichi. Hao watu je?"

t) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
u) Fafanua mbinu mbili za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo (alama 4)
v) Thibitisha kauli "Dunia ya msumari moto juu ya donda bichi" ukirejelea **Hadithi ya Mame Bakari.** (alama 6)
w) Fafanua jinsi mwanamke alivyosawiriwa katika hadithi hii. (alama 6)

**9. Tulipokutana Tena**

Nadhani kicheko chake kiliwaambukiza wenzangu maana vicheko vya nguvu viliwapasuka pamoja. Kama unavyoona, hivi vilikuwa vicheko vya mzaha na utani. Miongoni mwetu sote, Kazu alicheka zaidi. Alicheka kicheko mpaka mbavu zikamtafuna. Na alipocheka basi, alicheka kwa namna ya ajabu iliyonifurahisha sana. Alicheka huku ameviringa ngumi mbele ya kinywa kama ambaye anazuia hicho kicheko chenye nguvu za kutoa ***mwangwi*** uliosafiri robo dunia. Isitoshe, alipocheka namna hiyo, alijirusharusha kitini na kujivuta nyuma kwenye mgongo wa kiti na kuinua miguu yake mpaka soli za viatu vyake zikaonekak. Kumtazama Kazu akicheka ni namna ya kituko. Kila siku nikiwa


FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181

naye, mimi huhakikisha kwamba namchekesha kwa mzaha huu na ule ili nimwone namna anavyocheka. Hata hivyo, yeye naye hakuwa mchekeshaji mdogo.

“Aaa, hadithi za kichawi Kazu, ziko kila pahala duniani,” nilimwambia kwa kujitetea. “Unakumbuka mkasa maarufu hapa penu wa chatu lililotambaa kutoka Mashariki hadi Magharibi huku limemeza maelfu ya watu tumboni? Lilisafiri kwa masafa ya zaidi ya kilomita mia tano hivi na kuwatema watu hao huko Magharibi!”

**Maswali**

h. Tambua mbinu **tano** za kimtindo katika dondo hili. (alama 5)

i. Eleza jinsi mwandishi alivyofaulu kutumia mbinu rejeshi katika kuijenga hadithi ya Tulipokutana Tena. (alama 5)

j. Onyesha umuhimu wa mandhari ukirejelea Club Pogopogo. (alama 4)

k. Hakiki matatizo aliyoyapitia Bogoa Bakari aushini mwake. (alama 6)



FOR MARKING SCHEME CALL SIR ABRAHAM 0729125181